



TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA  
Kitalu Na. 339, Mtaa wa Nyerere - Kilimani  
S.L.P 1049, DODOMA/ 285, ZANZIBAR  
Simu: +255 734 047 775/734 119 978; (24) 2230494 (ZNZ)  
Barua Pepe: [info@chragg.go.tz](mailto:info@chragg.go.tz); [zanzibar@chragg.go.tz](mailto:zanzibar@chragg.go.tz)  
Tovuti: [www.chragg.go.tz](http://www.chragg.go.tz)

---

Desemba 3, 2021

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### **Tamko la THBUB wakati wa maadhimisho ya siku ya kimataifa ya watu wenye ulemavu, Desemba 3, 2021**

---

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) inaungana na wadau wote wa Kimataifa, Kikanda na Kitaifa wa utetezi wa haki za Watu Wenye Ulemavu kwa kuadhimisha **Siku ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu** Desemba 3, 2021.

Siku hii ni matokeo ya Azimio Na. 47/3, 1992 la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lililopitisha Desemba 3 ya kila mwaka kuwa ni siku ya maadhimisho ya Watu Wenye Ulemavu Duniani. Lengo la siku hii ni kuhamasisha jamii katika nchi husika kutambua haki, fursa sawa na ushiriki wa Watu Wenye Ulemavu katika masuala ya maendeleo, mahitaji yao, changamoto zinazowakabili na kutafuta namna ya kukabiliana nazo.

Kwa kuwa Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa, Serikali ina wajibu wa kutekeleza Azimio hilo kwa vitendo. Kitaifa maadhimisho haya kwa mwaka huu yanafanyika mkoani Tanga chini ya kauli mbiu isemayo: **“Wezesha uongozi na ushiriki wa watu wenye ulemavu katika Dunia jumuishi, fikivu na endelevu baada ya janga la UVIKO 19”** (*Leadership and participation of persons with disabilities towards an inclusive, accessible and sustainable post –COVID 19*).

Kwa kuzingatia kauli mbiu hii, THBUB inatambua jitihada za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kulinda na kutetea haki za Watu Wenye Ulemavu nchini. Serikali zote mbili zimeendelea kuboresha majengo ya Umma na kuwa rafiki kwa Watu Wenye Ulemavu, uwezeshaji kiuchumi kwa Watu Wenye Ulemavu na kuteuliwa katika nafasi mbalimbali za uongozi.

Serikali zote mbili zimeendelea kukemea na kuchukua hatua kwa mtu au watu wanaobainika kufanya vitendo vya ukatili, ubaguzi, unyanyasaji na unyanyapaa dhidi ya Watu Wenye Ulemavu. Katika kipindi hiki cha janga la UVIKO 19 Serikali zimechukua hatua mbalimbali kuwakinga Watu Wenye Ulemavu na athari ya ugonjwa huu. THBUB inazipongeza Serikali zetu kwa kuchukua jitihada za kulinda na kutetea haki za Watu Wenye Ulemavu.

Pamoja na mafanikio hayo, Watu Wenye Ulemavu wamekuwa wakikabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo kutumika kiuchumi kama ombaomba kwa maslahi ya watu wengine; ukatili; na kuendelea kuwepo kwa imani, mila, desturi na mitazamo potofu katika jamii dhidi ya Watu Wenye Ulemavu.

Hivyo, THBUB inapendekeza yafuatayo:

1. Serikali ziendeele na juhudi za kuwatambua Watu Wenye Ulemavu na mahitaji yao ili kuwawekea mazingira mazuri kupitia mfumo wa uwezeshaji kiuchumi waweze kujitegemea;
2. Wananchi waachane na imani, mila na desturi potofu dhidi ya Watu Wenye Ulemavu;
3. Wananchi watoe taarifa kwa mamlaka husika juu ya vitendo vya ukatili, ubaguzi, udhalilishaji na unyanyasaji dhidi ya Watu Wenye Ulemavu.

4. Wadau wote waungane pamoja na kutoa elimu kwa jamii ili kuhakikisha fursa na haki za Watu Wenye Ulemavu zinalindwa, zinakuzwa na kutetewa nchini.

***“Wezesha uongozi na ushiriki wa watu wenye ulemavu katika Dunia jumuishi, fikivu na endelevu baada ya janga la UVIKO 19.”***

Imetolewa na:



Mohamed Khamis Hamad  
**Makamu Mwenyekiti**

**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

Desemba 3, 2021